# Eastern Africa Journal of Contemporary Research (EAJCR)



**Uhusiano kati ya Asasi ya Familia na Uongozi wa Jamii katika Riwaya za *Kiswahili Dunia Yao (Mohamed 2006)* na *Kidagaa Kimemwozea (Walibora 2012)***

Justus Kyalo Muusya, Kitula King'ei, Richard M. Wafula

## Article information:

To cite this Article:

Muusya, J. K., King'ei, K., & Wafula, R. M. (2019). Uhusiano kati ya Asasi ya Familia na Uongozi wa Jamii katika Riwaya za Kiswahili *Dunia Yao (Mohamed 2006)* na *Kidagaa Kimemwozea (Walibora 2012). Eastern Africa Journal of Contemporary Research*, 1(1), 34-43.

## For Authors

If you would like to publish your conceptual/theoretical and empirical research articles, case studies and book reviews with EAJCR, please use for authors information about how write your work and submission guidelines. Please, visit http:// www.eajcr.org/for-authors/

## About Eastern Africa Journal of Contemporary Research (EAJCR)

The Eastern Africa Journal of Contemporary Research (EAJCR) (ISSN 2663-7367) is both an online (open access) and print double-blind peer-reviewed quarterly journal published by the Directorate of Research and Publications of Gretsa University, Kenya.

EAJCR aims at advancing the frontiers of knowledge by publishing contemporary multidisciplinary conceptual/ theoretical and empirical research articles as well as case studies and book reviews

# Uhusiano kati ya Asasi ya Familia na Uongozi wa Jamii katika Riwaya za Kiswahili za *Dunia Yao (Mohamed 2006)* na *Kidagaa Kimemwozea (Walibora 2012)*

**Justus Kyalo Muusya**
*Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya*
*Emeli: muusyaj@yahoo.com*

**Kitula King'ei**
*Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya*
*Emeli: gkkingei@yahoo.com*

**Richard M. Wafula**
*Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya*
*Emeli: wafula.richard@ku.ac.ke*

## Ikisiri

*Asasi ya familia ndio msingi wa kila jamii. Uongozi wa familia kwa hivyo huweza kupiga mwangwi uongozi wa jamii nzima. Huku ni kusema kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya namna familia zinavyoongozwa na uongozi wa jamii pana. Inakisiwa kuwa viongozi wengi wa jamii huwa na familia. Hii ina maana kuwa iwapo viongozi hawa wataweza kuongoza familia zao vyema kwa kuzingatia amali na maadili yatakiwayo, basi suala hili litajitokeza katika kiwango cha kitaifa. Na ikiwa viongozi watapotoka kimaadili katika kuzielekeza familia zao, basi upotovu huu utajitokeza katika uongozi wao wa jamii katika kiwango kingine. Makala haya yanalenga kuchunguza ikiwa katika riwaya za Kiswahili kuna uhusiano katika namna ambavyo familia zinaongozwa kwa upande mmoja na uongozi wa jamii kitaifa kwa upande mwingine. Utafiti awali unaonyesha kuwa kiongozi anayeshindwa kukuza na kuongoza familia yake ipasavyo huweza kushindwa vilevile kuongoza jamii katika ngazi za juu. Inakisiwa kuwa hii ni kwa sababu kiongozi huyo huwa amepotoka kimaadili. Kwa misingi hii, kiongozi ambaye anazingatia maadili bora, maadili hayo yataweza kujitokeza katika kiwango cha kifamilia sawa na kiwango cha kitaifa. Je, tunaweza kukisia mienendo ya kiongozi wa dola kwa kutathmini namna anavyoongoza familia yake? Je, tunaweza kubashiri uongozi wa familia ya kiongozi kwa kutathimini matendo yake katika ngazi ya kitaifa? Haya ni baadhi ya maswali ambayo tumeyajibu katika uchunguzi huu. Kwa hivyo, lengo la makala haya ni kuchunguza ikiwa makisio haya ni kweli au si kweli. Data ya utafiti huu ilikusanywa katika riwaya mbili zilizoteuliwa katika uchunguzi huu. Hizi ni Dunia Yao (Mohamed 2006) na Kidagaa Kimemwozea (Walibora 2012). Uchunguzi huu uliongozwa na nadharia ya daindamano. Hii ni nadharia ya kutathmini maadili ya viongozi katika jamii.*

**Istilahi Muhimu:** Asasi ya Familia, Uongozi wa Jamii, Dola, Daindamano na Maadili.

## 1. Utangulizi

Familia ni kundi la watu wanaoishi pamoja na ambao wana uhusiano ama wa kuzaliwa au wa ndoa. Familia huwa mhimili muhimu wa jamii yoyote ile. Hii ndio maana Mbiti (1975:175) anasema kuwa mahusiano yote katika jamii huanza katika familia. Anaongeza kuwa, kila mtu

katika jamii ya Kiafrika huwa sehemu ya familia. Kwa sababu hii, ni wazi kuwa familia ndio msingi wa uongozi wa jamii. Katika jamii ya Kiafrika, kiongozi alipaswa kuwa mtu aliye na umri mkubwa katika familia husika. Aghalabu alipaswa kuwa baba. Kiongozi yeyote awaye, muhimu ni kuwa asasi ya familia ikiwa na uongozi dhabiti, jamii nzima itakuwa dhabiti pia kwa vile hupiga mwangwi namna uongozi wa kitaifa ulivyo.

Nayo katiba ya Kenya (2010) inatambua familia kama kitengo asili na cha kimsingi katika mpangilio wa jamii. Kila mwanajamii hutarajiwa kuwa sehemu ya familia fulani. Mpangilio huo unahusisha uongozi wa jamii. Hii ina maana kuwa ubora wa uongozi wa kila jamii hutegemea uimara wa familia. Wakati huo huo Mwita (2018) anaeleza kuwa kuna mmomonyoko wa maadili katika mataifa ya Afrika katika viwango mbalimbali vya uongozi familia ikiwapo. Anahoji kuwa chanzo cha mmomonyoko huo ni rushwa, wizi, ubadhirifu wa mali ya umma, udanganyifu, unyanyasaji, ubaguzi kati ya mambo mengine. Kwa maoni yake, vitendo hivi vimeweza kuendelea hata ingawa serikali na vyombo vya usalama vimekuwa vikipigania kuvidhibiti. Vitendo hivi vya kuvunja sheria huweza kuwa na madhara mengine.

Dola nayo ni taasisi inayoendesha utawala wa nchi. Huweza vilevile kuelezwa kama nchi, serikali, taifa au utaratibu wa kisiasa wa jamii katika eneo fulani. LHRC (2013) inaeleza kuwa, taasisi hii ya dola huhodhi mamalaka ya aina tatu ambayo ni mamlaka ya utawala, bunge na mahakama. Nao Hallinger na Heck (2002) wanaeleza kuwa jukumu kuu la dola ni kusaidia watawaliwa wake kuwa na mtazamo sawa kuhusu malengo na maazimio ya kikundi hicho. Katika makala haya tumechunguza uhusiano kati ya kiongozi yeyote wa dola na familia yake. Mathalani, kiongozi wa familia anatarajiwa kuzingatia haki kwa watu wote wa familia yake bila kumbagua yeyote kwa misingi yoyote ile. Hii ina maana kuwa idara zote za dola na jamii kwa jumla zinatarajiwa kutekeleza sheria pasipo upendeleo wa aina yoyote. Idara hizi ni pamoja na kikosi cha askari na mahakama.



## 1.1 Nadharia ya Daindamano

Hii ni nadharia changamano yenye umahuluti wa mitazamo miwili ya daintolojia na umaandamano. Istilahi ya daindamano imeundwa kwa kuunganisha sehemu *dain* ya neno daintolojia na *ndamano* ambayo ni sehemu ya neno umaandamano. Ili kuweka bayana mawazo ya daindamano, tumefafanua dhana ya daintolojia na ile ya umaandamano.

### 1.1.1 Dhana ya Daintolojia

Katika falsafa ya amali na maadili katika jamii ya leo daintolojia ni mtazamo unaohusu matendo na maamuzi yanayohitajika kimaadili, yanayokatazwa na yale yanayoruhusiwa. Mhasisi wake ni Immanuel Kant. Wanafalsafa wengine ambao walichangia mawazo haya ni pamoja na Ross, Spranca, Ockham na Descartes.

Hawa wanashikilia kuwa mtu hawezi kulaumiwa kwa kusababisha maafa iwapo mtu huyo alibadilisha mkondo wa hatari iliyokuwa inawaelekea watu wengi hivi kwamba sasa itawaathiri wachache (Thomson, 1985). Lakini ikiwa mtu huyu ndiye alisababisha hatari au mkondo kama huu, atalaumiwa kwa kusababisha maafa – hata kama ataanzisha hatari hiyo kudhuru wachache na kwa kufanya hivyo awe ameokoa walio wengi (Foot, 1967; Thomson, 1985). Kwa misingi hii, kiongozi haruhusiwi na mtazamo huu kutumikisha watu anaowaongoza bila idhini yao hata

kama kwa kufanya hivyo mtu huyo analeta manufaa kwa watawaliwa wengine. Wanadai kuwa ni haki ya mtu kutotumiwa na mtu mwingine kwa manufaa ya anayemtumia. Kwa misingi hii basi ni kunyume cha haki mtu kutumiwa na mwingine bila idhini yake. Hata hivyo, kuna wanaodai kuwa kwa kutozuia maafa ambayo ulikuwa na uwezo wa kuzuia kwa urahisi ni jambo la kulaumiwa (Bennett, 1981). Naye Schaffer (2012) anaunga mkono maneno hayo kwa maoni kuwa kutozuia ni aina moja ya kusababisha.

Wanadaintolojia hushikilia kuwa kanuni za maadili hutawala hadi kiwango fulani – ambacho ni kilele. Kilele hiki kikipitwa huwa kanuni za daintolojia hazitumiki tena. Kwa hivyo umaandamano huchukua jukumu hili (Moore, 1997). Ieleweke kuwa kilele tunachozungumzia hapa huweza kubadilika kiviwango kutegemea kiwango cha matendo maovu yanayotendeka. Lakini wanavyohoji Ellis (1992) na Alexander (2000) ni shughuli ngumu sana ya kuonyesha mpaka wa kilele hiki ni upi au uko wapi. Mtazamo huu huweza kukizana na ule wa umaandamano. Hata hivyo, wajibu wa kimsingi ni kuwa watendee watu wengine matendo ambayo wao wenyewe wameyakubali na kuyaruhusu. Kulingana na Kant kitu cha kipekee kisichofikia daraja ya kuitwa kizuri ni nia njema (Kant, 1785). Kant anamaanisha kuwa nia yoyote njema ni sharti itekelezwe ili iwe na manufaa kwa wanajamii.

**1.1.2 Dhana ya Umaandamano**

Mtazamo huu hushikilia kuwa maamuzi na matendo yanapaswa kutathminiwa kwa misingi ya matokeo yanayoyatoa. Hivyo, wanaumaandamano hupaswa kuanza kwa kuonyesha umuhimu wa matokeo ya mambo, yanayoitwa kwa jumla mema. Kutokana na haya, ndio huwa wanaweza kusema kuwa maamuzi ya kutenda matendo hayo basi yanafaa kimaadili kuruhusiwa. Kwa misingi hii, kutathmini wema hutangulia maamuzi yanayofaa kimaadili.



Hata hivyo, wanaumaandamano huweza kutofautiana kwa mapana kuhusu kile ambacho basi wanapaswa kusema ndio wema. Nozick (1974) anaeleza kuwa wanaumaandamano hushikilia kuwa kutenda au kutotenda mambo fulani kwenyewe ndiko huweza kuitwa wema. Kuwa, ni jinsi wema unavyotandazwa miongoni mwa watu. Vilevile kuna wale wanaochukulia kuwa kando na kutenda wema miongoni mwa watu, jaribio la kufikia wema zaidi iwezekanavyo ndilo lengo la maamuzi na matendo ya watu. Hivyo, tendo linafaa kutendwa iwapo litahakikisha kiwango cha juu zaidi cha wema.

Mtazamo huu hupigwa kwa jinsi ambavyo unaruhusu mambo fulani maovu kuwatendekea watu wasio na hatia kama vile mauaji, kupigwa, kunyimwa mali na mengineo kwa nia ya kujaribu kupata manufaa na wema kwa wengine walio wengi. Hivyo, matokeo huweza kuhalalisha kitendo, maafa na mengine bora yawe yana manufaa kwa walio wengi. Kwa mujibu wa Slote (1984) baadhi ya wafuasi wa mtazamo huu hukwepa kudhihirisha kilele cha wema lakini huhakikisha kiwango fulani cha lazima cha wema kimefikiwa. Iwapo ni jukumu la mtu fulani kuwahudumia wengine, kisha iwe kuwa mtu huyo akilazimisha wengine wamsaidie kutoa huduma hiyo itatolewa vyema zaidi, basi suala hili litaruhusiwa kwa misingi ya mtazamo huu kwani matokeo ya kitendo husika yatakuwa makubwa. Kwa mfano, daktari wa upasuaji anaweza kuamua kumuua mtu mwenye afya njema ili amtoe viungo vitano tofauti ambavyo ataviweka kwa wagonjwa tofauti ambao wanavihitaji. Kwa kufanya hivyo, wagonjwa hawa wataweza kupona japo mmoja ambaye hakuwa mgonjwa atakufa.

### 1.1.3 Umahuluti wa Daintolojia na Umaandamano

Wasomi wenye maoni ya kushirikisha mitazamo hii miwili wanasema kuwa njia nzuri ya kuweka vipengele hivi pamoja ni kuupa kila mtazamo nafasi na majukumu yake yaliyo bayana na ambayo hayaingiliani na majukumu ya mtazamo ule mwingine (Nagel, 1986). Nao Lyons (1965) na Alexander (1985) wanahisi kuwa umaandamano huelekea kuangukia kuabudu kanuni hata pale ambapo matokeo ya maamuzi na matendo yangekuwa bora zaidi bila kutumia kanuni zozote aslani. Maoni haya ndio msingi wa kuasisiwa kwa nadharia ya daindamano.

Kwao, matendo mabaya ni matendo mabaya tu. Mabaya kwa Y na mabaya kwa X hayawezi kujumuishwa ili kupata mabaya makubwa zaidi. Hii ni kwa sababu kama anavyodai Taurek (1977) kati ya Y na X hakuna yule ambaye atakuwa amepatwa na jumla ya mabaya hayo. Lakini swali ni je, madai haya yanamaaanisha kuwa hakuna haja ya kuua mmoja kuokoa watano? Kama vifo vya watano havitajumuishwa ni kusema kuwa havitakuwa vifo vikubwa kuliko kifo cha mtu mmoja?

### 1.1.4 Mihimili ya Nadharia ya Daindamano

1. Mhimili mkuu wa nadharia hii ni kuwa huwa inakataza maamuzi na matendo maovu kwa watu wasio na hatia lakini iwapo kwa kuwadhuru wachache wengi watanufaika yanaweza kuruhusiwa.
2. Maamuzi na matokeo fulani hayawezi kuthibitishwa kwa matokeo ya kitendo hata yawe mewa kimaadili namna gani, hivyo maamuzi na matendo mengine hayakubaliwi kabisa.
3. Matendo mazuri ndiyo hupewa umuhimu wa kwanza katika wema. Matendo haya ni yale ambayo ni jukumu la mtu kuyatenda na yale asiyostahili kutenda.
4. Maadili ni uchaguzi wa mtu binafsi. Inachukuliwa kuwa ni matokeo tunayonuia kupata pamoja na njia za kuyafikia matokeo hayo au njia za kutenda tuyatendayo.

Nadharia hii ilitumiwa kueleza maadili ya viongozi wa familia na wale wa dola katika riwaya za Kiswahili za kisasa. Iliongoza kuhakiki ikiwa matendo ya viongozi huambatana na kanuni na matarajio ya wanajamii wanaoongozwa au la.

## 2. Uchunguzi wa Uhusiano Kati ya Asasi ya Familia na Uongozi wa Jamii

### 2.1 Uongozi katika Asasi ya Familia katika *Dunia Yao*

Katika *Dunia Yao* (2006), changamoto katika familia zimebainishwa. Mfumo wa familia ya Kiafrika umegeuka na hivyo kuathiri uongozi wa familia vibaya. Mtima akiwa Uingereza alijua fika kuwa wazazi wake walikuwa hawasemezani (Mohamed, 2006:8). Ugomvi wao ulitokana na mabadiliko katika taasisi ya ndoa na katika familia. Babake Ndi- alikataa kabisa kukubali kuwa mkewe alikuwa na uwezo wa kufanya kazi na kukimu familia yake hasa baada yake kufutwa kazi. Alidai kuwa mkewe alikuwa anashiriki ukahaba. Anakikataa chakula kilichochumwa na mkewe. Suala hili lilipelekea kuathirika vibaya kwa familia hii. Hata Ndi- amewahi kuwazia kujiua kutokana na mawazo haya. Naye Yungi, bintiye Ndi- upande mwingine anadai uhuru wake kwa nguvu. Anamfahamisha babake kuwa wasichana katika ujirani wao walikuwa wamepewa uhuru. Naye alikuwa ni sharti awe huru kufanya atakavyo na mwili wake (Mohamed, 2006:24). Anaongeza kuwa maisha yalikuwa yamebadilika kiasi kuwa watoto walikuwa na nafasi ya kuongoza na kuendesha familia zao, ikiwepo kuichumia riziki.

Yungi anamkumbusha babake kuwa udhibiti wa familia aliokuwa ameuzoea na aliokuwa anautaka hangeupata tena (Mohamed, 2006,25). Babake alikuwa hajazoea hali ambapo mtoto msichana alikuwa na usemi katika familia kiasi cha kuchelewa kurejea nyumbani. Jambo hili Ndi- alilipinga kabisa.

Binti mwingine wa Ndi- aliyeitwa Kilua naye anamwambia babake kuwa mamake hakushiriki ukahaba kama alivyodhania. Aliitafutia familia yake riziki kwa kufanya kazi ya kuuza chakula cha mchana kwenye ofisi. Alikuwa ni sharti aichumie familia yake kwa vile mumewe alikuwa ameshindwa kufanya hivyo baada ya kufutwa kazi. Huku ni kusema kuwa Kilua japo alikuwa mdogo kwa umri, alikuwa na nafasi kubwa ya kutoa maoni ya kuelekeza familia yake ikiwa ni pamoja na kumshauri babake. Imani ya kuwa mume ndiye mchumi kwa familia yake ndiyo iliyomwathiri vibaya Ndi- (Mohamed, 2006:90). Babake kwa kukubali mabadiliko haya, angekuwa anakubali kuwa uongozi taratibu ulikuwa unahamia kwa wanawake. Kutokubali huku ndiko kulimtia matatani hadi akafutwa kazi (Mohamed, 2006:91). Kufutwa kazi kwake kulikuwa balaa kwa familia yake. Alishindwa kuipatia riziki na akashindwa kumwelimisha Yungi. Zaidi, Kilua alionyesha uongozi bora katika familia yake. Alimjali babake alipogomea chakula cha mamake kiasi cha kumwibia chakula na kumwekea. Uadilifu wake huu ulilipwa na uovu. Alibakwa na kakake Jitu, unyama uliotamatisha maisha yake (Mohamed, 2006:198).

### 2.2 Uongozi wa Asasi ya Dola katika *Dunia Yao*

Katika *Dunia Yao* tunaona watu wasiokuwa na hatia wakiumizwa mno (Mohamed, 2006:195). Ndi- alikamatwa na kufungwa kwa tuhuma za kumuua mwanawe Jitu, kosa ambalo hakuwa amelitenda. Aliweza kufungiwa jela ya wendawazimu kwa vile hivyo ndivyo alifikiriwa. Hata hivyo, matendo yake ya uadilifu ndiyo yalimfanya aitwe mwendawazimu. Aliyekuwa ametekeleza uovu huo alikuwa bintiye, Yungi. Huyu ndiye alikuwa amemuua kakake Jitu akijaribu kumwokoa Kilua alipokuwa anabakwa na Jitu. Hata hivyo, hakuweza kuadhibiwa kwa vyovyote vile. Adhabu ilimwegemea baba mtu (Mohamed, 2006: 202-203).



Mohamed kwenye *Dunia Yao* anaendelea kuonyesha viongozi walikuwa wanajilimbikizia mali nyingi kutokana na uporaji wa raslimali za umma. Jamii ikawa na matajiri wachache na maskini wengi. Mali ambayo ingefaa wengi ikawa inahodhiwa na wachache. Jambo hili lilifanya uongozi kushindwa kukimu mahitaji ya kimsingi ya watu wake. Watu hao ambao ni maskini sasa wakawa wanafurika kwa viongozi hawa kuomba msaada wa chakula. Wakawa wa kung'ang'ania msaada usiowatosha. Wenyewe wakawa hawatambui kuwa msaada huo ni mali yao ambayo ingekuwa imeboresha maisha yao. Taasisi zote na asasi za jamii zikadidimia na kuwa mbaya kabisa. Elimu ikazorota kiasi kuwa mitihani ilikuwa ya kuuzwa kotekote. Mwandishi anaeleza hivi:

> *Jeshi la masikini hupanga mlolongo langoni kwa tajiri mkubwa kabisa wa nchi hii kungojea sadaka ya senti tano. Tajiri fulani anaiibia nchi na kisha kuzunguka na kuikirimu utumbo. Kisha kuna kukosa mkate. Nyumba nzima kukumbwa na malaria… hospitali mabanda. Makaburi ya umma. Madaktari wachache… shule mazizi ya mbuzi. Hazina vikalio wala vifaa.* (Mohamed, 2006:41-2).

Mohamed anahisi kuwa jamii haipaswi kuishi tu bila kujali amali na maadili ya viongozi wao.

Vilevile katika *Dunia Yao* umma ulichukua sheria mikononi mwao kwa kuwapiga vibaya kiasi cha kuwaua waliowakosea kama vile wizi. Wizi kama huu unaathiri familia kwa vile familia zinapoteza mali yake. Vyombo vya dola vingetarajiwa kuhakikisha usalama wa kutosha. Hakika ulikuwa ni mfumo wa uvunjaji sheria. Walijua kuwa vyombo vya dola vingejikokota mno kuona kuwa haki imefuata mkondo wake. Hivyo wakawa wanajipatia haki kwa kuvunja sheria zaidi (Mohamed, 2001:132). Aidha, Yungi alipompeleka nduguye Jitu katika kituo cha polisi kwa kuuza bidhaa zake za nyumbni, walevi wenzake waliwapa polisi hongo ili wamwachilie Jitu. Naye Ndera anakamatwa na polisi na kutupwa katika gari lao kama mzoga. Huku hayo yakiendelea, Ndera alimwambia Ndi- kuwa wamegundua njama yake ya kutaka kufyeka kuku wote. Alisema kuku akirejelea watu wote wenye mamlaka waliowadhulumu wengine. Ndera alikuwa tayari amemuua bwanamkubwa mmoja aliyemshuku kuikalia pensheni yake baada ya kutoka kazini. Hapa utovu wa maadili mema unazaa uongozi mwovu katika jamii. Uongozi huu unawaumiza watu wanaoongozwa huku nao wakijihami kwa uovu zaidi katika hatua za kulipiza kisasi (Mohamed, 2006:154). Sadala anashukiwa kukamatwa na kufungwa miaka mingi alipopatikana katika uwanja wa ndege katika nchi nyingine akisafirisha madawa ya kulevya. Mwandishi anadokeza kuwa polisi katika nchi hii nyingine walikuwa wanawajibikia majukumu yao hasa kuhusiana na matumizi ya madawa haya. Hata hivyo, kinyume chake ni kuwa taifa hili la akina Sadala lilipuuza msuala haya, au likaunga mkono ulanguzi wa mihadarati.

### 2.3 Asasi ya Familia katika *Kidagaa Kimemwozea*

Mtemi Nasaba Bora alijihusisha na mapenzi nje ya ndoa. Alijipatia wapenzi chungu nzima, wengine wakiwa wasichana wadogo kwa umri kama vile Lowela. Jambo hili lilimwathiri vibaya mke wake na watoto. Kwa mfano, Mashaka akiwa na umri mdogo aliweza kujiingiza katika mapenzi ya kiholela kama babake. Uhusiano wake na Ben Bella unapovunjika, anatokea kuwa mwendawazimu. Baadaye anamfumania mkewe na Amani chumbani chao cha kulala na moja kwa moja akampa talaka. Mwanawe mwingine, Madhubuti aliweza kumuasi babake kutokana na tabia na miendendo yake potovu (Walibora, 2012:87-88). Aliweza kupiga hatua hata ya kujitambulisha kwa jina la mamake na baadaye akahamia kwenye kibanda alichokuwa anaishi Amani, mkamaji wao. Hii ina maana kuwa uongozi potovu wa familia hii uliifanya isambaratike. Suala hili linatabiri uongozi mwovu wa Mtemi Basaba Bora katika jimbo la Sokomoko.



Nayo familia ya Mwalimu Majisifu iliathiriwa na changamoto kadha. Kwanza, watoto wake wote walikuwa walemavu. Jambo hili lilipelekea kushamiri kwa migogoro na hali ya kutoelewana kati yake na mkewe. Kila mmoja wao akimlaumu mwenzake kwa kuzaa watoto kama hao. Hata watoto wenyewe hawakuweza kufaidi utajiri wa baba yao (Walibora, 2012:30). Ulevi uliokithiri wa Majisifu ulikuwa suala lingine. Mara kwa mara waligombana kwa sababu ya ulevi huu kwa vile ulimfanya Majisifu asiweze kufaa mkewe kwa vyovyote katika kazi za nyumbani. Ulevi na utepetevu huu unajitokeza katika kiwango cha kitaifa namna ambavyo anafanya kazi mbalimbali ikiwepo ile ya kufundisha.

Babake Majisifu na Nasaba Bora aliiongoza vyema familia yake kwa misingi ya mafundisho ya kidini. Aliwaelekeza wanawe wawe na ushirikiano kila mara. Kila jioni aliwasomea Biblia na kuwashauri. Alihakikisha kuwa wameweza kupata elimu bora. Baadaye aliweza kuaga

dunia japo wakati huu wana wake hawa walikuwa wamekwishakuwa watu wazima. Kilichofuata ni watoto hawa kuanza kupuuza amali za kijamii. Waliweza kutengana na kuwa maadui. Majisifu aliyekuwa mpenda dini alitazamiwa kuwa kasisi kumrithi babake lakini aliweza kujitosa katika taaluma tofauti na hatimaye akawa mlevi chakari. Familia iliyokuwa na msingi bora ikapotoka kimatendo baada ya kiongozi wake kung'atuka.

### 2.4 Uongozi wa Asasi ya Dola katika *Kidagaa Kimemwozea*

Katika *Kidagaa Kimemwozea* Mtemi Nasaba Bora anapuuza matarajio ya jamii katika kuongoza jimbo la Sokomoko. Alikuwa anafanya maamuzi yenye mapendeleo kila mara. Kwa sababu hii, aliweza kuwadhulumu wengi. Hii ndio maana mwandishi anasema hivi:

> *Ni kesi ngapi alizoamua Bwana Mtemi Nasaba Bora kwa upendeleo na udhalimu? Neno lake lilikuwa ndilo sheria na asemalo ndilo liwalo. Bali watu walifyata ulimi* (Walibora 2012:52).

Aliweza kuwatuma askari wakampokonye mamake Imani shamba lake na kulifanya lake. Aliweza vilevile kufanya njama ya kuuliwa kwa babu yake Amani, Chichiri Hamadi ili atwae shamba lake kubwa. Aliweza vilevile kumfungisha jela Yusufu, mwanawe Hamadi. Huyu alifungwa maisha ili asije akadai shamba la babake au hata kuchunguza kifo cha baba mtu. Zaidi ni kuwa, katika kufungwa kwake Yusufu, alisingiziwa kuwa ndiye muuaji wa babake. Tunaelezwa hivi:

> *Mwenye shamba alikuwa tatizo na tishio kwa maendeleo ya Mtemi Nasaba Bora na kwa hiyo maendeleo ya nchi. Aliporejea nyumbani kutoka ng'ambo, Mtemi Nasaba Bora alikuwa tayari kamwandalia ufumbuzi wa kudumu* (Walibora 2012:13).



Mtemi huyu alikuwa miongoni mwa viongozi wengi wa Kiafrika walioiga maadili potovu ya Wazungu walipochukua hatamu za uongozi.

Matuko Weye aliweza kusimama kidete na kutetea haki ya umma. Japo alionekana mwendawazimu, alikuwa mwenye ujasiri mwingi. Bayana aliweza kusawiri madhila ambayo jamii yake ilipitia mikononi mwa viongozi dhalimu kama vile Nasaba Bora. Kwa wanajamii alikuwa kiongozi mwema. Hii ni kwa sababu kwa misingi ya nadharia ya dainamano, aliweza kudhurika kwa manufaa ya walio wengi. Kashfa yake kwa Mtemi hadharani ilimfanya akamatwe na kufungiwa seli duni. Japo aliumizwa na jambo hili, aliweza kuwazindua watu waone namna ambavyo waliweza kudhulumiwa, na hivyo wangejitolea katika kupingania uongozi bora (Walibora, 2012:71-72).

Mfumo mzima wa uongozi katika nchi ya Tomoko ulikuwa umepotoka. Viongozi wa mashinani walikuwa wanaiga kiongozi wa kitaifa katika kutekeleza mambo yao. Hii ndio maana mfumo huo unaendelea baada ya kifo cha Mtemi Nasaba Bora. Serikali ilituma kaimu Mtemi ambaye mwandishi anasema kuwa hotuba yake ya kwanza ilikuwa ya kawaida mno na kuwa wananchi walikuwa wamejitokeza kumlaki dikteta mpya. Hawangetarajia mabadiliko yoyote. Hii ndio maana walidai kuwa wangetaka Amani awe Mtemi. Ndiye walimwona kuwa na uwezo wa kuleta mabadiliko waliotarajia (Walibora, 2012:157). Hii tunaweza kuchukulia kuwa ni ishara tosha kuwa familia nyingi vilevile zilikuwa zimeathirika na kuvurugika mno.

Kikosi kizima cha walinda usalama kilikuwa kimepuuza mwenendo mwema utakiwao na jamii. Ili kujipatia kazi katika jeshi, mtu yeyote alikuwa ni sharti atoe hongo kwa wakuu wa kikosi hiki. Hongo hii ilikuwa inanufaisha wachache. Matokeo yake yalikuwa ni kuwafungia watu waliostahili kazi hii. Hivyo, wakichukuliwa wasiostahili utendakazi wao uliishia kuwa duni. Waliofaulu kwa hili ni watoto wa viongozi matajiri. Kwa mfano, Mtemi Nasaba Bora alikuwa amewapa hongo wakuu wa jeshi mwanawe Madhubuti apewe kazi katika kitengo cha wanahewa. Hili lilikuwa lifanyike bila mahojiano yoyote (Walibora, 2012:120). Hata hivyo, Madhubuti anaikataa kazi hii. Kwa kufanya hivyo, alikuwa anachangia kudumisha uwazi katika sekta hii. Huku ni kusema kuwa, uongozi usiokuwa na maadili bora katika familia ya Nasaba Bora ulikuwa unahamishiwa kwa jamii pana ya Wanasokomoko.

Hata hivyo, vikosi vya usalama vinatokea kugundua kuwa vilikuwa vinatumiwa vibaya na wakubwa wao na viongozi wa kisiasa, wakawa wanakataa baadhi ya amri waliopewa. Uzinduzi kama huu ni muhimu katika kusafisha uozo ulioko katika jamii. Katika mazishi ya Mtemi Nasaba Bora, askari walikataa kufyatua risasi 21 hewani kama ishara ya heshima kwa kiongozi huyo (Walibora, 2012: 160). Walikataa kwa vile walikuja kutambua kuwa alikuwa kiongozi mwovu na hivyo hakustahili heshima ya aina yoyote.

Viongozi katika jamii ya *Kidagaa Kimemwozea* wanapuuza uhuru wa sheria katika utendakazi wao. Mtemi Nasaba Bora alikosa kufuata sheria. Ajabu ni kuwa, mwenyewe kama kiongozi alitarajia watu aliowaongoza waweze kuzingatia sheria hizo. Kwa mfano, kulikuwapo na sheria ya kuwachanja mbwa kutokana na maambukizi ya magonjwa hatari. Alikuwa anawaadhibu watu katika jimbo la Sokomoko kwa kutochanja mbwa wao. Anapokumbushwa na mkewe kuwa mwenyewe hakuwachanja mbwa wake anakuwa mkali. Mkewe Bi Zuhura anamwambia namna hii:

> *Kumbuka tangu useme miaka nenda miaka rudi kwamba utawachanja hujawahi kuwachanja hawa mbwa wako. Mbwa hawa ni hatari kwa usalama. Na ni watu wangapi hapa Sokomoko uliowaadhibu kwa kutowachanja mbwa wao?* (Walibora 2012:104).

Maneno haya yanamsawiri Bi Zuhura, mkewe Nasaba Bora kuwa kiongozi mwenye kuzingatia maadili na amali za jamii. Alitambua umuhimu wa kuwachanja mbwa kwa vile mbwa asiyechanjwa alikuwa hatari kwa usalama wa watu wengine wengi.

Taasisi ya mahakama vilevile ilitumiwa na viongozi wenye maadili mabaya katika kutekeleza maovu yao. Kwa mfano, mahakama iliweza kuwahukumu vikali wananchi wasiokuwa na hatia hata chembe. Hii ni baada ya mahakimu kupewa hongo na matajiri ili matajiri hao waweze kujinufaisha kwa njia moja au nyingine kutokana na kifungo hicho. Mtemi Nasaba Bora aliweza kuwahonga mahakimu, polisi na hata makarani wa mahakama ili wamfunge Yusufu bila hatia. Lengo lake lilikuwa ni kuhakikisha hatatokea kudai shamba la marehemu babake Chichiri Hamadi ambalo Mtemi alikuwa amelinyakua. Nasaba Bora anamsimulia Amani alivyofanya:

> *Nilitaka kuwamaliza wote. Lakini watu niliowalipa kuitekeleza njama hawakufuata maagizo vema. Ikawa lazima kutafuta njia ya kumfungisha jela kwa kumnasabisha na*

> *mauaji ya babake. Ilibidi kulipa hela nyingi za kadhongo, kuwalipa polisi, makarani wa mahakama, majaji, wajua tena mti hauendi ila kwa nyenzo* (Walibora, 2012:150).

Hata hivyo, baadaye Mtemi Nasaba Bora anabadilika. Aliweza kueleza uovu wake mwenyewe. Ndipo akaandika ushahidi kwenye barua wa kumtoa lawamani Yusufu. Hivyo, kesi kuhusu Yusufu inaanzishwa upya na wanaharakati wa kutetea haki. Hawa walikuwa ni pamoja na Amani na Madhubuti (Walibora, 2012:155). Hii ilikuwa ishara ya kufunguliwa na kuachiliwa huru kwa wafungwa wengi wasiokuwa na hatia waliofungwa kimakosa. Mahakama inaonekana kubadilika na kuanza kuzingatia sheria na haki katika utendakazi wake.

## 3. Hitimisho

Katika makala yetu, tumeweza kuchunguza na kuonyesha kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya uongozi wa familia na uongozi wa taifa. Tumeweka wazi namna ambavyo uongozi wa familia unaweza kutumiwa kubashiri namna ambavyo kiongozi wa familia ataweza kuongoza katika kiwango cha kitaifa. Vivyo hivyo, tunapopatana na kiongozi katika kiwango cha kitaifa tunaweza kukisia namna ambavyo anaiongoza familia yake. Hii ina maana kuwa kiongozi aliyepotoka kimaadili katika kiwango cha kitaifa ataweza vilevile kudhihirisha maadili hayo katika familia yake. Makisio yetu hapa yalikuwa kwamba kiongozi mwenye maadili bora huweza kudhihirisha maadili yayo hayo katika uongozi wake kwenye viwango mbalimbali katika jamii. Ni wazi kuwa sio uongozi pekee unaoathiri familia. Kifo cha kiongozi kinaathiri uongozi wake pia. Aidha, tunaona kuwa uongozi wa kitaifa unaathiri familia pale ambapo kiongozi wa dola ananyang'anya familia ardhi yao. Jambo ambalo linapelekea kusambaratika kwa familia hiyo. Wakati huo huo, kwa misingi ya nadharia yetu ya Daindamano, huu ni uongozi uliokosa maadili mema. Hii ni kwa sababu ardhi ya wanajamii wengi inatwaliwa na mtu mmoja, hivi kwamba anajinufaisha yeye huku walio wengi wakiumia. Hivyo, uongozi wa dola uliopotoka huweza kuathiri jamii nzima hadi kiwango cha familia nyingi, hata bila ya kiongozi wa familia hizi husika kupotoka kimaadili.



Mohamed anaelekea kuunga mkono uongozi wa wanawake na watoto katika jamii. Anaonekana kutoa maoni kuwa wakati umefika ambapo wanaume wanapaswa kukubali uongozi wa wanawake na watoto katika viwango vyote ikiwa ni pamoja na uongozi wa familia. Kulingana naye, wanawake wakiwa viongozi watazingatia maadili ya kijamii zaidi kuliko wanaume. Hivyo, Mohamed anaashiria kuwa uongozi wa wanaume aghalabu hupuuza amali za kijamii na maadili yatakiwayo. Hata hivyo, ameweka wazo kwamba sio jambo rahisi wanawake kuchukua hatamu ya uongozi kwa vile wanaume huchukulia kuwa uongozi wa jamii nzima kutoka kiwango cha kifamilia hadi kiwango cha kitaifa ni hifadhi yao. Kwa sababu hii, wanawake na vijana hawana budi kujifunga kibwebwe kutwaa mamlaka hayo kwa nguvu. Upande mwingine, Walibora anasawiri kuwa uongozi wa jamii nzima, ikiwepo familia unapaswa kubakia mikononi mwa wanaume. Kwamba wanawake wanapaswa kuongozwa katika viwango vyote kuanzia katika kiwango cha kifamilia. Hata hivyo, Walibora anatambua kuwa wanaume ni watovu wa maadili katika uongozi wao. Kwa maoni yake, viongozi waliopotoka kitabia na kimienendo wanapaswa kujiasa na kuadilishwa na wanajamii wanaowaongoza ndipo waweze kubadilika ama wakajiondoa wenyewe mamlakani.

## Marejeleo

Alexander, L. & Ferzan (2009). *Crime and Culpability: A Theory of Criminal Law*. Cambridge: CUP.

Bennett, J. (1981). "Morality and Consequences," in *The Tanner Lectures on Human Values Vol. 2*, S. McMurrin, (ed.). Cambridge: Cambridge University Press.

Fox, D. R., and Prilleltensky, I. (1997). *Critical Psychology. An Introduction.* London: Sage.

Gramsci, A. (1971). *Prison Notebooks.* New York: International Publishers.

Kant, I. (1785) *Groundwork of the Metaphysic of Morals,* H.J. Paton, trans., New York: Harper and Row, 1964.

Mohamed, A. S. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.

Moore, M. (2008). Patrolling the Borders of Consequentialist Justifications: The Scope of Agent-Relative Obligations. *Law and Philosophy*, 27(1), 35–96.

Nozick, R. (1974). *Anarchy, State and Utopia*. New York: Basic Books.

Oomen, T. (2001). Recognizing Multiple Modernities. A Prelude to Understanding Globalization. http//members.com/oommen.html. (last visited 15-07-2011.

Schaffer, J. (2012). Disconnection and Responsibility. *Legal Theory*, 18, 399–435.

Scheffler, S. (1982). *The Rejection of Consequentialism*. Oxford: Oxford University Press.

Sen, A.K. (1982). Rights and Agency. *Philosophy and Public Affairs*, 11(1): 3–39.

Slote, M.A. (1984). *Common-Sense Morality and Consequentialism*. London: Routledge.

Wafula, R. M. na K. Njogu (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Nairobi JKF.

Walibora, K. (2012). *Kidagaa Kimemwozea*. Nairobi: Target Publications Limited.